**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE**

**SHULE YA SEKONDARI KAFULE**
**S.L.P 09,**
**ILEJE-SONGWE**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule 0768332311**
**Makamu Mkuu wa Shule 0766748127**
**Matron 0769030831**
**Patron 0759699746**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAFULE HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE MKOA SONGWE MWAKA…………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka Julai……………na atasoma tahasusi mojawapo kati ya hizi zilizopo hapa shuleni kulingana na alivochaguliwa ambazo ni **HGK,HGL,HGFa** na **HGLi**

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari Kafule ipo Mkoani Songwe wilaya ya Ileje KM 63 kutoka makao makuu ya wilaya. Ukitoka Mbeya panda magari yanayoenda Tunduma shuka standi ya Mpemba ukitoka Dar Es Salaam panda magari yanayoenda Tunduma au Sumbawanga na ushike Mpemba, kadhalika kama unatoka njia ya Sumbawanga panda magari yanayokwenda Mbeya kisha shuka mpemba.

Toka Mpemba utapata magari yanayokwenda Isoko kuanzia saa 2:00 mpaka saa 4:00 Asubuhi magari hayo yanaenda moja kwa moja isoko ambako ndo mwisho wa kituo cha mabasi kinachopatikana na shule ilipo. Mjulishe kondakta kuwa wewe ni Mwanafunzi unaekwenda shule ya Sekondari Kafule nae atakushushia kituo sahihi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe itakayotangazwa na Serikali. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kwa tarehe itakayopangwa na Wizara(**OWM-TAMISEMI**)

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

**SARE ZA SHULE**

**A. WAVULANA**

- **i.** Suruali moja rangi ya khaki na ya pili rangi ya bluu bahari pamoja na tai ndefu 2 za rangi blue bahari na khaki
- **ii.** Mashati mawili(2) ya rangi nyeupe kitambaa cha tetroni yenye mikono mirefu na mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto
- **iii.** Sweta rangi ya kijani kibichi (kuna baridi ya wastani)-Ukikosa huko unaweza kupata jirani na shule kwa Ths.10,000
- **iv.** Viatu vyeusi vya kamba kisigino kifupi jozi mbili na soksi nyeupe jozi mbili.Kwa msaada zaidi tazama picha za sare hapo chini.

**B. WASICHANA**

- i. Sketi mbili(2) moja rangi ya khaki na ya pili rangi ya bluu bahari pamoja na tai ndefu 2 za rangi bluu bahari na khaki
- ii. Blauzi 2 za rangi nyeupe kitambaa cha tetroni yenye mikono mirefu na mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto.
- iii. Sweta ya rangi ya kijani kibichi (kuna baridi ya wastani)- Ukikosa huko unaweza kupata jirani na shule kwa Tsh.10,000
- iv. Viatu vyeusi vya kamba kisigino kifupi jozi mbili na soksi nyeupe jozi mbili.

Kwa msaada zaidi tazama picha za sare hapo chini

**VITU VYA KUZINGATIA KWENYE SARE**


**Kwa wavulana:**

- i) Upana wa mkanda wa suruali kiuno uwe inchi 2
- ii) Mifuko mitatu,miwili pembeni (wa kutoboa) nyuma mmoja upande wa kulia
- iii) Upana wa suruali chini uwe inchi 17 (*Zingatia maelekezo*)
- iv) Suruali iwe na turn up na marinda mawili.Hapo chini inaonesha rangi ya vitambaa husika.




**Kwa wasichana:**

i) Sketi iwe ndefu karibia na kisigino.
ii) Upana wa marinda uwe inchi **3** na yawe ya kupanga
iii) Zipu ikae upande wa kushoto wa sketi
iv) Upana wa mkanda wa kiunoni iwe inchi 2
**v)** Ziwe na mfuko mmoja upande wa kulia. Hapo chini inaonesha rangi ya vitambaa husika.




**SARE ZA MICHEZO**
**WAVULANA NA WASICHANA**

- Bukta 2 rangi ya bluu
- Fulana 2 rangi ya bluu
- Viatu vya michezo raba jozi 2
- Soksi ndefu rangi nyekundu josi 2



**BUKTA IAMBATANE NA FULANA YA BLUU**

**RANGI YA HIJABU**
Wanafunzi wa kike wa kiislamu watavaa hijabu rangi nyeupe.

**NGUO ZA KUVAA BAADA YA VIPINDI VYA DARASANI NA SIKU ZA MAPUMZIKO**
**WASICHANA**

- Truck suit bluu bahari –Ukikosa huko unaweza kupata jirani na Shule kwa Tsh.20,000**.**
- Gauni la drafti nyeupe na bluu bahari lenye marinda ya kupanga
- T-shirt rangi ya kijivu-Ukikosa huko unaweza kupata jirani na Shule kwa Tsh.15,000



**GAUNI** **TRUCK SUIT** **T-SHIRT YA KIJIVU**

**WAVULANA**

- Truck suit rangi ya bluu bahari na mistari myeupe-Ukikosa huko unaweza kupata jirani na Shule kwa Tsh.20,000
- Suruali rangi ya bluu mshono kama sare ya shule
- T-shirt yangi ya kijivu –Ukikosa huko unaweza kupata jirani na Shule kwa Tsh.15,000



**TRUCK SUIT** **T-SHIRT YA KIJIVU** **SURUALI YA BULUU**

**MUHIMU**:

1. Mwanafunzi anaposafiri kuja shule avae sare ya shule.Mwanafunzi haruhusiwi kuja na mavazi tofauti na hayo(aliyoandikiwa katika barua yake ya kujiunga kidato cha Tano).
2. Maagizo ya mashono yaliyoagizwa yazingatiwe atakae kiuka maelekezo haya atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa mavazi hayo.

### 2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -

i. Madaftari **10**(Counter book Q3 AU 4)
ii. **Ream (A4)** za Karatasi Mbili (2) kwa mwaka-Ukikosa huko unaweza kupata karibu na Shule kwa Tsh.13,000
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Calculator;
v. Mathematical set 1
vi. Godoro liwe na vipimo vya futi 2½ **x 6 –**ukikosa huko unaweza kupata jirani na shule kwa Tsh.35,000.
vii. Mashuka Jozi 2 bluu bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. **HGK** waje na ndoo lita 10 (mbili), hard broom moja,soft broom moja, squizer moja na jembe lenye mpini.
ix. **HGL** waje na ndoo lita 10 (mbili), Shoka bila mpini, kwanja moja na panga.
x. **HGFa** na **HGLi** waje na ndoo 2 za lita 10, Hard broom moja,Soft Broom moja na Kifaa cha kudekia na ndoo yake (Mopper),

Soft broom,Hard broom,squizer na kwanja ukikosa huko unaweza kuvipata jirani na Shule kwa Tsh.4,500 kila kimoja.

## 2.2 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Zingatia:**

Kila mwanafunzi aje na michango ya Uendeshaji wa shule kiasi cha shilingi **80,000/=** na wanafunzi wasiyo na bima ya afya wanapaswa kuja na kiasi cha fedha Shilingi **50,400** kwa ajili ya Bima ya Afya.

Mchango wa **TSH.80,000** ilipwe kupitia Akaunti Namba **60801100003 NMB.** Jina la Akaunti ni KAFULE SECONDARY SCHOOL FUND.

**Angalizo:**Mwanafunzi atapokelewa shuleni ikiwa tu atakuwa amelipia michango hiyo yote na kuwasilisha lisiti ya malipo ya Bank**.**

## 3. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni**

**ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule** **DAUDI MWAKATOGA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KAFULE
S.L.P. 9
ILEJE

**NB: Hivi sasa kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi**

**husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0768332311**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0768603154**
- **Mwandamizi Taaluma 0759699746**
- **Mwalimu wa Afya 0754854355**

**SHULE YA SEKONDARI KAFULE**

**FOMU YA KUKUBALI**

**1.Sehemu ya mwanafunzi**

Mimi……………………………………………………………Ninaikubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza/tano………………katika shule ya sekondari ya kafule na nitafika shuleni bila kuchelewa.Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi.Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni…………………………………………………………….

……………………………………………………………………

……………………………………………………………………

……………………………………………………………………

……………………………………………………………………

**2.Sehemu ya mzazi/mlezi** Mimi……………………………………………....ninakubali mtoto wangu……………………………………….........kuchukua nafasi kuingia shule ya sekondari Kafule kidato cha…………Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na Shule wakati wote na kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni:-…………………………………………………………..

……………………………………………………………………….

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Saini…………………………………………tarehe……………………………………………

**SHULE YA SEKONDARI KAFULE**

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina langu kamili lilivyotumika kidato cha nne…………………………………………
   Dini yangu/dhehebu …………………………………...
2. Jina kamili la baba mzazi/mlezi…………………………………………………..kazi yake…………………………………..
   Anwani kamili ya baba mzazi/mlezi………………………………………..
   Namba yake ya simu ya mkononi…………………………………………..
   Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi…………………………………………
   Namba yake ya simu ya mezani……………………………………………
   Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi:
   Mkoa……………………Wilaya……………Tarafa…………………kata……………
   Kijiji/mtaa…………………………………
3. Jina kamili la mama mzazi/mlezi…………………………………………………..kazi yake…………………………………..
   Anwani kamili ya mama mzazi/mlezi………………………………………..
   Namba yake ya simu ya mkononi…………………………………………..
   Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi…………………………………………..
   Namba yake ya simu ya mezani……………………………………………
   Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi:
   Mkoa…………………Wilaya……………Tarafa…………………kata……………………
   Kijiji/mtaa…………………………………

**4.Majina ya watu wanne wanaoruhusiwa kumtembelea/kumchukua mtoto wako**

| Na | Jina lake | Uhusiano | Mahali anakoishi | Anuani na namba yake ya simu |
|---|---|---|---|---|
| 01 | | | | |
| 02 | | | | |
| 03 | | | | |
| 04 | | | | |

**5.Shule nilizosoma msingi hadi kidato cha nne**

| Na | Jina la shule | Darasa/kidato | Kuanzia mwaka hadi mwaka | Mkoa | Wilaya | Kijiji/Mtaa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | | | | | | |
| 02 | | | | | | |
| 03 | | | | | | |
| 04 | | | | | | |

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENTS**

**KAFULE SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.BOX 09,**
**ILEJE.**

**Date ………………**

**DISTRICT MEDICAL OFFICER**
**P.O.BOX…………………**
**…………………………………**
**Dear Sir/Madam**
**Re: A REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine………………………………………………………….as to his/her physical and mental fitness for admission as a form five student at Kafule secondary school in the year 2024

**Yours sincerely;**

**HEADMASTER**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KAFULE
S.L.P. 9
ILEJE

**The Headmaster,**
I have examined the student ………………………………………………………………. as shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary education.

1) Vision with/without glasses, Right…………………………………left………………………………
2) Blood pressure……………………………………..Hemoglobin……………………………………
3) Hearing…………………………………………………………………………………………………………
4) Urine(a)Albumen…………………………............(b)Sugar…….................................................
5) (a) Venereal diseases………………………………………. (b) Bilharzia……………………………………
6) Pregnancy………………………………………………………………………………………
7) Neurosis……………………………………………………………………………………………
8) Is there any abnormality of: - (a) The heart…………………………………………………….(b) Lungs………………………….............................................................................................

(c)The Spleen…………………………………………………………………………………

9)Are there any serious diseases e.g. Leprosy,epilepsy,asthma,diabetes etc…………………….
Any....Comments……………………………………………………………………………………………
…………………............................................................................................................

**Date: ……………………………………………………………………………………………….**

**Signature of Medical Officer………………………………………………………………...**

**Designation……………………………….................................................................**